# HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI YA WILAYA GAIRO MNAMO TAREHE 7/1/2022

**Wajumbe waliohudhuria:**

1. Isaya Mihinzo — Mwenyekiti
2. Salima Rajabu — Katibu
3. Dr. Godbless E. Luhanga — Mjumbe
4. Nivoneia E. Levery — Mjumbe
5. Adv. Waryoba Mussa — Mjumbe

**Wajumbe wasiohudhuria:**

1. Nurath Hussein - Kwa taarifa
2. Eunice M. Kyungay - Kwa taarifa

**Mjumbe Mualikwa:**

1. Mhandisi Felix Mbepi

**Sekretarieti:**

1. Fredrick Kiria

**AGENDA ZA KIKAO:**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma muhtasari wa bodi ya zabuni wa tarehe 20/12/2021
4. Kujadili mapendekezo ya timu ya manunuzi kwa ajili ya wakandarasi wa kutekeleza miradi ifuatayo kupitia mpango maalumu wa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVICO – 19 kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka shirika la fedha duniani;

i. Kujenga jengo la wagonjwa wa dharura (Emergence Medical Department) kwa bajeti ya shilingi 300,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/01.

ii. Kujenga nyumba ya watumishi (Tatu kwa moja) kwa bajeti ya shilingi 90,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/02.

5. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
6. Kufunga kikao

**AGENDA. NA TB/1/7/1/2022 - KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu aliwasilisha agenda na kumkaribisha mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 9.05 Alasiri.

**AGENDA. NA.TB/2/7/1/2022 - KUTHIBITISHA AGENDA**

Jumla ya agenda tano (5) ziliwasilishwa na kuthibitishwa. Agenda hizo ni;-

**AGENDA ZA KIKAO:**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma muhtasari wa bodi ya zabuni wa tarehe 20/12/2021
4. Kujadili mapendekezo ya timu ya manunuzi kwa ajili ya wakandarasi wa kutekeleza miradi ifuatayo kupitia mpango maalumu wa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVICO – 19 kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka shirika la fedha duniani;

i. Kujenga jengo la wagonjwa wa dharura (Emergence Medical Department) kwa bajeti ya shilingi 300,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/01.

ii. Kujenga nyumba ya watumishi (Tatu kwa moja) kwa bajeti ya shilingi 90,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/02.

5. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
6. Kufunga kikao

**AGENDA. NA.TB/3/7/1/2022: Kusoma muhtasari wa bodi ya zabuni wa tarehe 20/12/2021**

Katibu aliwasilisha agenda na kuwasilisha muhtasari wa tarehe 20/12/2021 kwa ajili ya wajumbe kuhakiki, wajumbe waliusoma muhtasari na kuthibitisha kuwa ni muhtasari sahihi na kusainiwa.

**AGENDA. NA.TB/4/7/1/2022: Kujadili mapendekezo ya timu ya manunuzi (PMU) kwa ajili ya wakandarasi wa kutekeleza miradi kupitia mpango maalumu wa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVICO – 19 kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka shirika la fedha duniani.**

Katibu wa Bodi ya Zabuni aliwasilisha agenda na kutoa maelezo kuwa mnamo tarehe 5/1/2022 wajumbe wa Timu ya tathmini waliwasilisha taarifa ya tathmini Kitengo cha Manunuzi na mnamo tarehe 6/1/2022 wajumbe wa Kitengo cha Manunuzi walifanya kikao cha kujadili taarifa

hiyo. Ufuatao ni mchanganuo wa mapendekezo ya timu ya tathmini, timu ya manunuzi(PMU) na wajumbe wa Bodi ya zabuni kuhusu zabuni zilizotangazwa kwa kutumia njia ya manunuzi ya ushindani kwa utoaji wa zabuni ulio na utaratibu maalum (Restricted method) mnamo tarehe 22/12/2021 na ufunguzi ulifanyika mnamo tarehe 29/12/2021 saa 5.00 Asubuhi katika ukumbi mdogo wa Halmashauri:

1. **Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura (Emergence Medical Department) lenye bajeti ya shilingi 300,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/01.**

Zabuni hii wakandarasi waliotakiwa kuomba ni wa daraja la nne(IV) na kuendelea wa ujenzi wa majengo hata hivyo wakandarasi waliopewa nyaraka za zabuni ni Taasisi za Serikali za ujenzi wa majeng, Kampuni binafsi za ujenzi wa majengo ambao walipatikana katika tovuti ya Bodi ya Wakandarasi ambao ni;

1. PACHA Construction – S.L.P 5230 – Morogoro
2. CSWS – Vikosi vya Ujenzi – S.L.P 879 – Dodoma
3. Suma JKT – S.L.P 105989 – Dar Es Salaam
4. NHC – S.L.P 2977 – Dar Es Salaam
5. MCB Co, ltd - MUST Mbeya – S.L.P 131 - Mbeya
6. Deep Construction ltd – S.L.P 1154 – Morogoro
7. Watumishi Housing – S.L.P 5119 – Dar Es Salaam
8. MACEA Construction – S.L.P 425 - Morogoro

Hata hivyo siku na muda wa ufunguzi ni wakandarasi watano (5) tu kati ya nane waliochukua nyaraka za Zabuni waliorejesha nyaraka za zabuni ambao ni;

1. PACHA Construction – S.L.P 5230 – Morogoro,
2. Suma JKT – S.L.P 105989 – Dar Es Salaam
3. NHC – S.L.P 2977 – Dar Es Salaam
4. MCB Co, ltd - MUST Mbeya – S.L.P 131 - Mbeya
5. MACEA Construction – S.L.P 425 – Morogoro

Mchanganuo wa gharama za wakandarasi na sababu za kutokuwa na sifa ya kuingia katika hatua ya tathmini ya kina ni kama ifuatavyo:

| Na. | Jina la Kampuni na anwani | Nchi ilikotoka Kampuni | Gharama ya mradi pamoja na VAT | Hati ya uwakilishi kisheria | Sababu ya kutokuwa na sifa ya kuingia katika hatua ya tathmini ya kina |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | NHC – S.L.P | Tanzania | Tshs | Amewasili | i. Makadirio ya gharama (Bills of |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2977 – Dar Es Salaam | | 890,140,025/= | sha | Quanties) zilizojazwa hazijasainiwa kikamilifu na mtu aliyepewa mamlaka ya kusaini nyaraka ya zabuni hiyo.<br>ii.Muda wa utekelezaji wa mradi ni miezi mitano (siku 150) badala ya miezi minne (siku 120).<br>iii.Gharama ya mradi aliyowasilisha ya shilingi 890,140,025/= imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 300,000,000.00 kwa asilimia 196.7%. |
| 2 | Suma JKT – S.L.P 105989 – Dar Es Salaam | Tanzania | Tshs 883,823,586.61 | Amewasilisha | i.Makadirio ya gharama (Bills of Quanties) hazijasainiwa kikamilifu na mtu aliyepewa mamlaka ya kusaini nyaraka ya zabuni hiyo.<br>iii.Gharama ya mradi aliyowasilisha ya shilingi 883,823,586.61 imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 300,000,000.00 kwa asilimia 194.6%. |
| 3 | PACHA Construction – S.L.P 5230 – Morogoro | Tanzania | Tshs 678,741,947.20. | Amewasilisha | i.Amewasilisha makadirio ya gharama (Bill of Quantities) yenye gharama ya shilingi 678,741,947.20.<br>ii. Gharama ya mradi aliyowasilisha ya shilingi 678,741,947.20 imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 300,000,000.00 kwa asilimia 126%. |
| 4 | MCB Co, ltd - MUST Mbeya – S.L.P 131 – Mbeya | Tanzania | Tshs 749,724,494/= | Amewasilisha | i. Makadirio ya gharama (Bills of Quanties) hazijasainiwa kikamilifu na mtu aliyepewa mamlaka ya kusaini nyaraka ya zabuni hiyo.<br>ii. Gharama ya mradi aliyowasilisha ya shilingi 749,724,494/= imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 300,000,000.00 kwa asilimia 150%. |
| 5 | MACEA | Tanzania | Tshs | Amewasili | i. Kampuni yake ina usajili wa Bodi ya wakandarasi daraja la tano la |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Construction - S.L.P 425 - Morogoro | 753,724,327.40 | sha | ujenzi wa majengo badala ya daraja la nne kama ilivyotakiwa katika tangazo.<br>ii.Gharama ya mradi aliyowasilisha ya shilingi 753,724,327.40 imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 300,000,000.00 kwa asilimia 151%. |

Mapendekezo ya wajumbe wa timu ya tathmini, wajumbe wa timu ya manunuzi (PMU) na wajumbe wa bodi ya zabuni kama ifuatavyo:-

| **Na** | **Zabuni namba** | **Maelezo ya zabuni** | **Mapendekezo ya timu ya tathimini** | **Mapendekezo ya timu ya manunuzi** | **Mapendekezo ya wajumbe wa bodi ya zabuni** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | LGA/143/2021/ 2022/BL/W/01. | Kujenga jengo la wagonjwa wa dharura (Emergence Medical Department) | Zabuni hii itangazwe tena kwa wakandarasi wa majengo waliosajiliwa daraja la sita na kuendelea (Class six and above) badala ya daraja la nne na kuendelea (Class four and above). | Mradi wa ujenzi wa jengo la dharura kwa bajeti ya shilingi 300,000,000.00 hata kama tangazo likirudiwa bado gharama itakuwa kubwa kwa sababu gharama ya vifaa vya ujenzi ipo juu. Pendekezo la wajumbe mradi huu usitangazwe tena ila utekelezwe kwa njia ya "Force Account" kwa maana vifaa vinunuliwe na kazi ya ujenzi ushindani | Pendekezo la wajumbe mradi huu utekelezwe kwa "Force Account" kwa maana vifaa vinunuliwe na kazi ya ujenzi ushindani ufanyike kwa Taasisi za Serikali na kampuni binafsi zilizoomba zabuni hii, wakandarasi wengine watakaojitokeza wenye sifa na "Local fundi's wenye sifa. Swala la usimamizi wa kazi kwakuwa bajeti ndogo hatuwezi kumwajiri msimamizi wa kazi hivyo ofisi ya ujenzi ijipange kusimamia mradi kwa kufuata taratibu zote.Pia kama Serikali itaona inafaa ni bora miradi hii iondolewe kodi kama |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ufanyike kwa Taasisi za Serikali na kampuni binafsi zilizoomba zabuni hii, wakandarasi wengine watakaojitokeza wenye sifa na "Local fundi's wenye sifa. Pamoja na kutumia njia hiyo fedha za kutekeleza mradi kiasi cha 300,000,000.00 ili itoshe Serikali itoe kodi katika mradi huu kwa maana katika ununuzi wa vifaa na fundi atakaejenga. Hata hivyo ofisi ya Ujenzi iandae makisio ya gharama ya vifaa na kazi zitakazofanywa na fundi kwa uhalisia ili makasio hayo | ilivyokuwa katika miradi ya maji iliyokwisha tekeleza kwa fedha za "Water Sector Development Programme – WSDP" |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | yapelekwe TAMISEMI. | |

2. **Ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Tatu kwa moja) yenye bajeti ya shilingi 90,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/02.**

Zabuni hii wakandarasi waliotakiwa kuomba ni wa daraja la saba (VII) na kuendelea wa ujenzi wa majengo hata hivyo wakandarasi waliopewa nyaraka za zabuni ni Taasisi za Serikali za ujenzi wa majengo, Kampuni binafsi za ujenzi wa majengo ambao walipatikana katika tovuti ya Bodi ya Wakandarasi ambao ni;

1. PACHA Construction – S.L.P 5230 – Morogoro
2. CSWS – Vikosi vya Ujenzi – S.L.P 879 – Dodoma
3. Suma JKT – S.L.P 105989 – Dar Es Salaam
4. NHC – S.L.P 2977 – Dar Es Salaam
5. MCB Co, ltd - MUST Mbeya – S.L.P 131 – Mbeya
6. Diocese of Morogoro Technical Support Co. Ltd – S.L.P 320 - Morogoro
7. Deep Construction ltd – S.L.P 1154 – Morogoro
8. Watumishi Housing – S.L.P 5119 – Dar Es Salaam
9. MACEA Construction – S.L.P 425 - Morogoro

Hata hivyo siku na muda wa ufunguzi ni wakandarasi watano (5) tu kati ya tisa (9) waliochukua nyaraka za Zabuni waliorejesha ambao ni:

1. PACHA Construction – S.L.P 5230 – Morogoro
2. Suma JKT – S.L.P 105989 – Dar Es Salaam
3. NHC – S.L.P 2977 – Dar Es Salaam
4. Diocese of Morogoro Technical Support Co. Ltd – S.L.P 320 - Morogoro
5. MACEA Construction – S.L.P 425 - Morogoro

Mchanganuo wa gharama za wakandarasi na sababu za kutokuwa na sifa ya kuingia katika hatua ya tathmini ya kina ni kama ifuatavyo:

| Na. | Jina la Kampuni na anwani | Nchi ilikotoka Kampuni | Gharama ya mradi pamoja na VAT | Hati ya uwakilishi kisheria | Sababu ya kutokuwa na sifa ya kuingia katika hatua ya tathmini ya kina |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Suma JKT – S.L.P 105989 – Dar Es Salaam | Tanzania | Tshs 265,883,051.60 | Amewasilisha | i. Makadirio ya gharama (Bills of Quanties) zilizojazwa hazijasainiwa kikamilifu na mtu aliyepewa mamlaka ya kusaini nyaraka ya zabuni hiyo. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Diocese of Morogoro Technical Support Co. Ltd – S.L.P 320 - Morogoro | Tanzania | Mkandarasi wakati wa ufunguzi aliwasilisha gharama ya shilingi 141,529,000.00 baada ya timu ya tathmini kuhakiki gharama ilikuwa shilingi 186,513,160/=.Hata hivyo mkandarasi huyo alitoa punguzo la asilimia 5% ya gharama (vifaa na ufundi vyenye gharama ya shilingi 158,062,000.00) sawa na punguzo la shilingi 7,903,100/= hivyo kufanya gharama ya kazi kuwa shilingi 178,610,060/= | Amewasilisha | |
| 3 | NHC – S.L.P 2977 – Dar Es Salaam | Tanzania | Tshs 273,764,309.00 | Amewasilisha | i. Makadirio ya gharama (Bills of Quanties)zilizojazwa hazijasainiwa kikamilifu na mtu aliyepewa mamlaka ya kusaini nyaraka ya zabuni hiyo. |
| 4 | MACEA Construction – | Tanzania | Mkandarasi wakati wa | Amewasilisha | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | S.L.P 425 – Morogoro | | ufunguzi aliwasilisha gharama ya shilingi 273,474,564.00, baada ya timu ya tathmini kufanya marekebisho gharama ilikuwa shilingi 272,419,643/= | | |
| 5 | PACHA Construction – S.L.P 5230 – Morogoro | Tanzania | Tshs 312,139,521.00 | Amewasilisha | i. Amewasilisha makadirio ya gharama (Bill of Quantities) yenye gharama ya shilingi 312,139,521.00<br>ii. Gharama ya mradi aliyowasilisha ya shilingi 312,139,521.00 imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 90,000,000.00 kwa asilimia 146.8%.ii. Gharama ya mradi ni shilingi 312,139,521.00 |

Baada ya uchambuzi wa awali Kampuni zilizokidhi vigezo na kuingia hatua ya tathmini ya kina ni zifuatazo:-

1. Diocese of Morogoro Technical Support Co. Ltd – S.L.P 320 – Morogoro
2. MACEA Construction – S.L.P 425 – Morogoro

**Mapendekezo ya wajumbe wa timu ya tathmini, wajumbe wa timu ya manunuzi (PMU) na wajumbe wa bodi ya zabuni kama ifuatavyo:-**

| **Na.** | **Zabuni namba** | **Maelezo ya zabuni** | **Mapendekezo ya timu ya tathimini** | **Mapendekezo ya timu ya manunuzi (PMU)** | **Mapendekezo ya wajumbe wa bodi ya zabuni** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | LGA/143/2021/ 2022/BL/W/02. | Ujenzi wa nyumba ya watumishi (Tatu kwa moja ) | **I.**Timu ya tathmini imempendekeza Mkandarasi Diocese of Morogoro Technical Support Co. Ltd – S.L.P 320 – Morogoro kutekeleza mradi huo kwa gharama ya shilingi 178,610,060/= kwa sababu gharama yake inamanufaa kwa mwajiri baada ya kutoa punguzo la asilimia 5% ya gharama ya vifaa na ufundi kama ilivyoelezwa hapo juu kwa masharti yafuatayo:- i.Kampuni iitwe | Mradi wa ujenzi wa nyumba ya watumishi (tatu kwa moja) kwa bajeti ya shilingi 90,000,000.00 hata kama tangazo likirudiwa bado gharama itakuwa kubwa kwa sababu gharama ya vifaa vya ujenzi ipo juu. Pendekezo la wajumbe mkandarasi kufanya nae majadiliano ili kupunguza gharama wakati gharama yake ni asilimia 98.45% ya bajeti ya mradi ni kitu kigumu katika kutekeleza mradi mbali ya kuwa na mapungufu mengine kama yalivyoainishwa.Hivyo wajumbe wamependekeza mradi utekelezwe kwa njia ya "Force | **Pendekezo la wajumbe** mradi huu utekelezwe kwa "Force Account" kwa maana vifaa vinunuliwe na kazi ya ujenzi ushindani ufanyike kwa Taasisi za Serikali na kampuni binafsi zilizoomba zabuni hii, wakandarasi wengine watakaojitokeza wenye sifa na "Local fundi's wenye sifa. . Swala la usimamizi wa kazi kwakuwa bajeti ndogo hatuwezi kumwajiri msimamizi wa kazi hivyo ofisi ya ujenzi ijipange kusimamia mradi kwa kufuata taratibu zote, ili kuondokana na hoja za ukaguzi.Pia kama Serikali itaona inafaa ni bora mradi huu uondolewe kodi kama ilivyokuwa katika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa ajili ya majadiliano ili kupunguza gharama kwasababu gharama imezidi bajeti ya mradi ya shilingi 90,000,000.00 sawa na asilimia 98.45% pamoja na kuwasilisha nyaraka zifuatazo:- a. Bank statement kadri ya mahitaji ya zabuni. b. Kuwasilisha nyaraka za ushahidi wa ukamilishaji wa kazi zinazofanana na aliyoomba. c. Kuwasilisha leseni ya biashara iliyo hai. d. Kuwasilisha sifa za taaluma na uzoefu za watumishi | Account" kwa maana vifaa vinunuliwe na kazi ya ujenzi ushindani ufanyike kwa Taasisi za Serikali na kampuni binafsi zilizoomba zabuni hii, wakandarasi wengine watakaojitokeza wenye sifa na "Local fundi's wenye sifa. Pamoja na kutumia njia hiyo fedha za kutekeleza mradi kiasi cha 90,000,000.00 ili itoshe Serikali itoe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika mradi huu kwa maana katika ununuzi wa vifaa na fundi atakaejenga. Hata hivyo ofisi ya Ujenzi iandae makisio ya gharama ya vifaa na kazi zitakazofanywa na fundi kwa uwalisia ili makasio hayo yapelekwe TAMISEMI. | miradi ya maji iliyokwisha tekeleza kwa fedha za "Water Sector Development Programme". |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | wake.<br>e. Kuwasilisha ushahidi wa umiliki wa vifaa vya kufanyia kazi kadri ya matakwa ya zabuni kulingana na mradi.<br>**II.**MACEA Construction – S.L.P 425 – Morogoro, timu ya tathmini haikumpendekeza kwasababu gharama yake ni kubwa ukilinganisha na bajeti ya mradi ya shilingi 90,000,000.00 hivyo gharama yake ilizidi kwa asilimia 202.7%. | | |

**AGENDA. NA.TB/5/7/1/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Katibu alisoma agenda na kumkaribisha Mwenyekiti. Ndipo Mwenyekiti alisema hakupokea mengineyo.

**AGENDA. NA.TB/6/7/1/2022: KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuchangia hoja mbalimbali katika kikao. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 10.45 Jioni.

**MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA KUTIWA SAINI NA:-**

Isaya Mihinzo .................................... Salima Rajabu ....................................

(Jina la mwenyekiti) (Jina la Katibu)

SAINI .................................... SAINI ....................................

TAREHE 27/01/2022 .................................... TAREHE 27/1/2022 ....................................